

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA THELATHINI NA SABA

31 MEI, 2023



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA THELATHINI NA SABA – TAREHE 31 MEI, 2023

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA NISHATI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

479. MHESHIMIWA JOSEPH MICHAEL MKUNDI (UKEREWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, nini mkakati wa Serikali katika kuboresha maslahi na mazingira ya kazi kwa Walimu ili kuwaongezea morali ya kazi.

480. MHESHIMIWA ENG. STELLA MARTIN MANYANYA (NYASA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Wodi katika Kituo cha Afya Kihangara.

481. MHESHIMIWA NJALU DAUDI SILANGA (ITILIMA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Madaraja katika Mto Garamoha, Isolo, Nyagokolwa, Mbogo na Mhuze Wilayani Itilima.

482. MHESHIMIWA LEAH JEREMIAH KOMANYA (MEATU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatekeleza ahadi ya ujenzi wa daraja la juu katika Mto Mwamanongu.

OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

483. MHESHIMIWA SOPHIA HEBRON MWAKAGENDA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, kwa nini Serikali inaajiri kwa kigezo cha Mwaka wa kumaliza Chuo na kupitia Mafunzo ya Jeshi.

484. MHESHIMIWA ENG. MWANAISHA NG'ANZI ULENGE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, lini Serikali itaweka wazi vigezo vya kubaini Kaya Maskini zinazostahili kupata msaada wa *TASAF*.

WIZARA YA KILIMO:

485. MHESHIMIWA JUSTINE LAZARO NYAMOGA (KILOLO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza tija katika uzalishaji wa zao la Pareto Wilayani Kilolo.

486. MHESHIMIWA ALLY JUMA MAKOA (KONDOA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji katika Kata ya Serya utaanza.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

487. MHESHIMIWA LUCY JOHN SABU (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, lini Serikali itaanzisha Benki ya Vijana Wajasiriamali.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

**488. MHESHIMIWA EMMANUEL PETER
CHEREHANI (USHETU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini Serikali itatenga maeneo ya malisho ya mifugo katika Pori la Usumbwa *Forest reserve*.

WIZARA YA MAJI:

**489. MHESHIMIWA ESTHER LUKAGO MIDIMU
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya Mradi wa Maji Sumve, Malya na Malampaka baada ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

**490. MHESHIMIWA NOAH LEMBURIS SAPUTU
(ARUMERU MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Serikali itafanya ukarabati wa Mnada wa Ng'ombe na Mbuzi wa Olokii.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA NISHATI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

DODOMA
31 MEI, 2023

N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE

